**Environmental Management and Biodiversity Conservation of Forests, Woodlands, and Wetlands of the Rufiji Delta and Floodplain**

# Mafunzo Kwa Wanavijiji Kuhusu Sheria Zinazohusu Usimamiaji Wa Maliasili Kwa Jamii

(VIJIJINI, WILAYA YA RUFIJI, MKOA WA PWANI)

3 – 19 MEI, 2001

# Volume 2 of 2 - Swahili Main Report

**Dr. H. Majamba, T. Macha na E. Mshana.**




**Technical Report No. 21**

**July 2001**

**For more information please contact**

Project Manager,
Rufiji Environment Management Project
P O Box 13513
Dar es Salaam, Tanzania.
Tel: 44 Utete Rufiji or 73731 / 0811 322366 Dar es Salaam
Email: rempute1@bushmail.net or iucndar@epiq.or.tz

[1] The Rufiji District Council implements Rufiji Environment Management Project with technical assistance from IUCN – The World Conservation Union, and funding from the Royal Netherlands Embassy.

## Rufiji Environment Management Project – REMP

**Project Goal:** To promote the long-term conservation through 'wise use' of the lower Rufiji forests, woodlands and wetlands, such that biodiversity is conserved, critical ecological functions are maintained, renewable natural resources are used sustainably and the livelihoods of the area's inhabitants are secured and enhanced**.**

**Objectives**

- To promote the integration of environmental conservation and sustainable development through environmental planning within the Rufiji Delta and Floodplain.
- To promote the sustainable use of natural resources and enhance the livelihoods of local communities by implementing sustainable pilot development activities based on wise use principles.
- To promote awareness of the values of forests, woodlands and wetlands and the importance of wise use at village, district, regional and central government levels, and to influence national policies on natural resource management.

**Project Area**

The project area is within Rufiji District in the ecosystems affected by the flooding of the river (floodplain and delta), downstream of the Selous Game Reserve and also including several upland forests of special importance.

**Project Implementation**

The project is run from the district Headquarters in Utete by the Rufiji District Administration through a district Environmental Management Team coordinated by the District Executive Director. The Project Manager is employed by the project and two Technical Advisers are employed by IUCN.
Project partners, particularly NEMC, the Coast Region, RUBADA, The Royal Netherlands Embassy and the Ministry of Natural Resources and Tourism, collaborate formally through their participation in the Project Steering Committee and also informally.

**Project Outputs**

At the end of the first five –year phase (1998-2003) of the project the expected outputs are:
An Environmental Management Plan: an integrated plan for the management of the ecosystems (forests, woodlands and wetlands) and natural resources of the project area that has been tested and revised so that it can be assured of success - especially through development hand-in-hand with the District council and the people of Rufiji.

Village (or community) Natural Resource Management Plans: These will be produced in pilot villages to facilitate village planning for natural resource management. The project will support the implementation of these plans by researching the legislation, providing training and some support for zoning, mapping and gazettement of reserves.

Established Wise Use Activities: These will consist of the successful sustainable development activities that are being tried and tested with pilot village and communities and are shown to be sustainable

Key forests will be conserved: Forests in Rufiji District that have shown high levels of plant biodiversity, endemism or other valuable biodiversity characteristics will be conserved by gazettement, forest management for conservation, and /or awareness-raising with their traditional owners

# Shukrani

Ripoti hii isingeweza kukamilika bila ushirikiano na msaada wa watu kadhaa wakati wa mafunzo. Tungependa kutoa shukrani zetu kwa Rose Hogan, Albert Jimwaga, Barnabas, Dr.Olivier, Mrema, Ndali, Chaugambo na Mpili Kassim wote wa MUMARU kwa ushirikiano na msaada wao.

Pia tungependa kuwashukuru wafanyakazi wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ambao tulienda nao vijijini – Revocatus X.L. Nandi (Mipango ya Matumizi ya Ardhi – Kilimo), Pili A. Mwambeso (Kilimo), Zuhura Rashid (Afisa Maendeleo ya Jamii), Fortunatus Ndasi (Idara ya Elimu na Utamaduni) Juma Mkungura – Ohii (Afisa Wanyamapori Msaidizi wa Wilaya), Phillipo Kilonzo (Afisa Misitu) Hussein H. Gamalieli (Afisa Kilimo), Saidi Sagara (Afisa Uvuvi), John Eniyoye (Afisa Wanyamapori wa Wilaya) na Bwenda I. Bainga (Afisa Kilimo). Heather Hoag pia alitupa moyo na alitupatia maoni ya maana yaliyotusaidia kutengeneza vipindi vya mafunzo katika vijiji vya Twasalie na Jaja.

Mwisho lakini si haba, tungependa kushukuru kwa ukarimu wa wanavijiji katika vijiji vyote vinne na walimu wa Mbunjumvuleni kwa kutupatia ushirikiano wote muhimu. (Majina ya wanavijiji waliohudhuria kwenye vijiji vyote yameorotheshwa kwenye kiambatanisho “B” ya Ripoti hii)

# Yaliomo

**Shukrani** ..... **i**
**Yaliomo** ..... **ii**
**1 Chimbuko** ..... **1**
**2 Utangulizi** ..... **2**
**3 Timu ya Watoa Mafunzo** ..... **2**
**4 Utaratibu Wa Ufundishaji** ..... **3**
**5 Ripoti Ya 'Field'** ..... **5**
5.1 Kijiji Cha Twasalie (Delta) ..... 5
5.2 Kijiji Cha Jaja (Delta) ..... 7
5.3 Kijiji Cha Mtanza Msona ..... 8
5.4 Kiji Cha Mbunju Mvuleni Na Vitongoji Vya Mpima na Mupi ..... 9
**6 Ufupisho wa Mafunzo kwa Ujumla** ..... **11**
**7 Viambatanisho** ..... **12**
7.1 Kiambatanisho 'A' ..... 12
7.2 Kiambatanisho 'B' ..... 14
7.3 Kiambatanisho 'C' ..... 20
7.4 Mapicha ..... 22

# 1 Chimbuko

Katika kuitekeleza sera ya serikali kuhusu utunzaji maliasili kwa kuwashirikisha wananchi kuweza kutunza maliasili zilizopo kwenye maeneo yao, Timu ya Wanasheria wa Mazingira (LEAT) waliingia mkataba na Mradi wa Usimamizi wa Mazingira Rufiji (MUMARU) ili kutengeneza, kutoa na kuandika kozi ya mafunzo kuhusu sheria za utunzaji maliasili zinazoendana na vijiji katika vijiji vilivyochaguliwa katika wilaya ya Rufiji, Mkoa wa Pwani. LEAT na MUMARU waliingia mkataba ulioanza tarehe 30 April 2001 hadi 15 Juni 2001.

Lengo na madhumuni ya mafunzo haya kimsingi ni kuongeza ufahamu wa wanavijiji na uelewa wa sheria za utunzaji maliasili kwa ujumla lakini hasa kwenye zile sheria zinazohusu maliasili zinazopatikana katika maeneo yao. Kozi pia iliandaliwa katika hali ya kuweza kuhakikisha kwamba wanavijiji wananaweza kutengeneza sheria ndogondogo kufuatana na utaratibu uliowekwa kisheria ili kutunza vizuri maliasili zao.

Itakuwa busara, katika sehemu hii ya ripoti, kutoa ufafanuzi wa mtazamo na maoni yetu kuhusu viwango vya uelewa vya wanavijiji kabla ya kuanza vipindi vya mafunzo.

Kiwango cha uelewa wa wanavijiji kuhusu mambo ya mazingira kwa ujumla kilikuwa kinaridhisha. Katika vijiji vingi, wanavijiji wanajua aina za mazingira na maliasili zilizopo katika vijiji vyao na umuhimu wa kuhifadhi mazingira na maliasili hizo. Katika kila kijiji, walikuwa ni wanavijiji wenyewe waliochora ramani za vijiji vyao wakionyesha sehemu maliasili zinapopatikna. Pia wametengeneza mipango na mikakati ya kuhakikisha kwamba maliasili zinatumika kwa manufaa yao na kuwaletea maendeleo zaidi. Vijiji vyote vimeunda Kamati za Magingira ambazo wajumbe wake wameandaa taratibu zilizowasilishwa kwenye katana na kupitishwa. Hata hivyo, taratibu hizi haziko katika mfumo unaokubalika kupitishwa ili kuzifanya ziwe sheria ndogondogo.

Isipokuwa katika kijiji kimoja (Twasalie), ambacho kwa mlingano na vijiji vingine kipo nyuma, kwa wastani uwezo wa wanavijiji kufuatilia na kuelewa mafunzo yaliyotolewa ulikuwa wa kuridhisha. Hakika, kama mtazamo wa viongozi wa kijiji (na wazee) wa Twasalie hautabadilika kuwawezesha wanavijiji wengi zaidi kushiriki katika kufikia maamuzi, basi itakuwa ni vigumu kutekeleza mipango ya usimamizi wa mazingira na maliasili na taratibu walizojiwekea katika kuhifadhi mazingira na maliasili zilizopo kijijini.
Katika vijiji karibu vyote, wanavijiji walikuwa na uelewa wa umuhimu wa kuwa na sheria kusimamia matumizi ya maliasili katika vijiji vyao. Hata hivyo, hawakuwa na ufahamu wa kutosha wa hatua muhimu za kufuata ili kuweka utaratibu wa kisheria ili kufikia lengo hili la matumizi bora ya maliasili.

Mara nyingi hata hivyo, wanavijiji wengi hawakuonekana kuzijua haki na wajibu wao dhidi ya mawakala wa utekelezaji wa sheria na watu kutoka nje ya vijiji vyao katika usimamizi na matumizi kwa ujumla ya maliasili katika vijiji vyao kama zilivyoainishwa katika sheria husika.

# 2 Utangulizi

Mafunzo yalifanyika katika vijiji vinne (Twasalie, Jaja, Mbunju/ Mvuleni na Mtanza/Msona) vilivyopo katika Wilaya ya Rufiji lakini vyenye masuala mbalimbali na yanayotia changamoto ya kisheria yanayohusiana na utunzaji wa maliasili. Wanavijiji katika vijiji hivi pia walikuwa na tofauti za utamaduni, uzoefu wa kijamii ambao ulikuwa na vikwazo kwa kozi ya mafunzo.

Makundi ya walengwa kimsingi yalikuwa wanavijiji katika serikali za vijiji, kamati za utunzaji wa maliasili za kijiji, skauti wa maliasili wa kijiji na watendaji wa kata. Mara nyingi, hata hivyo, wanavijiji wengine, ambao hawakuwa kwenye ngazi za uongozi wa kijiji walialikwa na walishiriki kikamilifu katika vipindi vya mafunzo.

MUMARU imekuwa ikijihusisha na usimamizi wa mazingira katika tambarare na delta ya mto Rufiji. Imekuwa ikifanya kazi katika vijiji vinne vilivyochaguliwa kwa kozi ya mafunzo. MUMARU imewasaidia wanavijiji kuandaa na kuunda vikundi vya mipango ya utunzaji wa mazingira vilivyopewa kazi ya kuelekeza maendeleo ya mipango ya utunzaji mazingira ya kijiji.

Kisha wanakijiji waliijadili mipango hiyo katika mabaraza ya vijiji na yakapitishwa. MUMARU pia iliandaa vipindi vya mafunzo kwa wanavijiji katika vijiji hivi vinne ili kuwapa wanavijiji uelewa wa jumla (msingi) katika nyanja nyingine zinazohusiana na maliasili kama vile kilimo na mifugo, misitu na ufugaji nyuki, utunzaji wanyamapori na uvuvi.

Wakiwa wameshapewa nyenzo muhimu katika kutunza maliasili katika ardhi zao, vijiji viliweka njia za kuhakikisha kwamba mipango hiyo inatekelezwa ipasavyo. Kati ya njia ambazo wanavijiji waliziweka ni kutengeneza kanuni kadhaa zilizoambatana na adhabu.

Iligundulika baadaye, wakati wa mafunzo kwamba kwa wanavijiji wengi kanuni hizi zilikuwa zimelengwa kufanya kazi kama sheria ndogondogo. Iligundulika pia kwamba kwa wanavijiji wengi, nyingi ya “sheria” hizi zilikuwa zina mapungufu kwa kuwa utelekelezaji wake dhidi ya baadhi ya watenda makosa katika matukio kadhaa ulijidhihirisha kuwa mgumu.

Wanavijiji, wao wenyewe, waliyataja mambo ya kisheria yanayohusu haki na wajibu wao katika kutunza maliasili katika maeneo yao na waliwaomba MUMARU wawasaidie kuwapata walimu wa kuwapa mafunzo ya muda mfupi. MUMARU waliitikia wito huo wa wanavijiji na wakawapa LEAT kazi hiyo ya kutoa mafunzo ya sheria kwa wanavijiji.

Ripoti hii inatoa ufupisho wa mafunzo kwa maoni ya walimu/watoa mafunzo.

# 3 Timu ya Watoa Mafunzo

Kwa kuzingatia mkataba kati ya MUMARU na LEAT, LEAT iliunda timu ya watoa mafunzo ambayo iliwashirikisha wanachama watatu wa LEAT. Wanachama hawa ni:

1. Dr. H. I. Majamba (Kiongozi wa timu)
2. Bw. Ebenezer Mshana; na
3. Bw. Theo Macha

# 4 Utaratibu Wa Ufundishaji

Baada ya kuelezwa kwa ufupi kwamba kundi la walengwa wa mafunzo linahusisha watu ambao ni wa elimu ya chini, utaratibu wa ufundishaji uliotumika ulikuwa ni wa muda mfupi, uliozingatia ubadilikaji wa mara kwa mara na ambao ulikuwa wa maswali ya kuweza kujua asili ya matatizo ambayo kila kijiji kilikuwa nayo.

Utaratibu wa ufundishaji uliotumika ulikuwa ni wa mahojiano ya pande mbili: watoa mafunzo na wanavijiji. Tulichagua sheria husika za kujadiliwa na tukachambua masuala ya kisheria ya kutilia mkazo kutokana na mambo yaliyowasilishwa na wanavijiji wenyewe. Hatukuwa na utaratibu ulioandaliwa kabla kwa sababu mazingira na mambo ya kujadiliwa kwa kila kijiji yalikuwa tofauti.

Tuliutumia kwa makusudi utaratibu wa kufundisha taratibu, tukiuliza maswali na katika kufanya hivyo tukaweza kupata mambo yaliyoonekana hayajaeleweka vizuri kwa nia ya kuyatolea ufafanuzi baadaye. Utaratibu huu wa ufundishaji ulikuwa muhimu kwa sababu watoa mafunzo walihitaji kujua masuala yenye matatizo ili kutoa mapendekezo yanayopatikana katika sheria.

Pia tulitumia utaratibu wa kufanya mazoezi ya maswali baada ya kila kipindi au mwishoni mwa vipindi vyote kwa kutegemea uelewa wa wanakijiji. Tuliwagawanya wanavijiji katika makundi na kuliuliza kila kundi kujalidili maswali yaliyotolewa na wao kwa pamoja. Kupitia kwa mwakilishi wa kundi husika, waliwasilisha majibu yao katika kipindi cha uwasilishaji ambapo wote walishiriki katika kujadili. Walijibu maswali katika chati kubwa. Hii iliwapa watoa mafunzo nafasi ya kuyaelezea zaidi maeneo/mambo ambayo yalionekana hayajaeleweka vizuri.

Utaratibu mzima wa kufundishia ulitumika katika vijiji vyote vinne unaweza kuandikwa kwa ufupi hapa chini:

### 4.1.1 Hatua ya I:

- Baada ya kutambulishana na ufunguzi rasmi wa mafunzo, wanavijiji walichora ramani za vijiji vyao zikionyesha mipaka na aina za maliasili ili kuweza kuweka msisitizo kwenye sheria zinazohusika. Wakati wa kuuliza maswali ya kutafuta ufafanuzi, watoa mafunzo pia waliweza kuyatambua matatizo ya kisheria yaliyopo.

- Kamati za Maliasili za Vijiji (zinajulikana kama Kamati za Mazingira katika vijiji vingine) zilitoa ufafanuzi wa Mipango yao ya Maliasili/Matumizi ya maliasili na mafanikio waliyoyapata. Katika kufanya hivyo, waliweza pia kuonyesha mapungufu na matatizo yaliyopelekea kushindwa kuyatatua matatizo hayo. Katika hatua hii, watoa mafunzo waliyaona mambo ya kisheria na mambo mengine ambayo ingawa hayakuwa ya kisheria moja kwa moja lakini yalikuwa na athari za kisheria ndani yao.

### 4.1.2 Hatua ya II:

Wanavijiji waliokuwa wanajua kusoma na kuandika walikuja na kalamu na karatasi. Katika baadhi ya vijiji, serikali za vijiji zilitoa makaratasi. Watoa mafunzo walitumia chati kubwa na wakati mwingine walitumia ubao na kusogea mahali ambapo kulihakikisha wanavijij wanaweza kuandika.

Watoa mafunzo walianza vipindi kwa kutoa muhtasari wa sheria kwa ujumla, wakiweka msisitizo katika:

1. ***Sheria Mama:*** Sheria zinazotungwa na Bunge ambazo zinatakiwa zitungwe kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Bunge au vinginevyo zinakuwa batili. Mamlaka ya Bunge kutoa uwezo wa kutunga sheria kwa mamlaka nyingine, taasisi na maafisa.
2. ***Katiba ya Nchi***: Wajibu wa kikatiba wa kila mwananchi kutunza maliasili za nchi, kazi ya utengenezaji/utungaji sheria iliyowekwa mikononi mwa Bunge.
3. ***Sheria Ndogondogo***: Sheria zinazotungwa na mamlaka/watu waliopewa mamlaka ya kufanya hivyo na Sheria Mama zikihusisha taratibu, na sheria ndogondogo. Sheria ndogondogo za vijiji za utunzaji wa maliasili zipo katika kundi hili. Zinahitaji kutoenda kinyume na maagizo yaliyowekwa na Sheria Mama au vinginevyo zitakuwa batili.
4. ***Kesi za Kimahakama***: Msisitizo uliwekwa na mifano ilitolewa kuonyesha jinsi kesi zilizoamuliwa na mahakama za juu zinavyoweza kuwa sehemu ya sheria. Kwa kuzingatia ugumu wa kushughulika na suala hili, watoa mafunzo walitoa ufafanuzi wa somo hili kwa kutoa mifano mbalimbali kwa kutumia nahau ambazo zingeweza kueleweka vizuri zaidi na kundi la walengwa.
5. Sheria ***za Kimila***: Taratibu mbalimbali zilizotokana na mila na desturi zilijadiliwa ambazo zilihusiana na utunzaji maliasili na ambazo zilikuwa moja kwa moja au sio moja kwa moja katika sheria. Mifano ilitofautiana kutoka kijiji hadi kijiji kutegemeana na hali ya maliasili na mila. Mara nyingi watoa mafunzo walijaribu kuwashirikisha wazee kutoa mifano ya taratibu (mila, desturi) ambazo ziliheshimiwa na watoa mafunzo walijadili jinsi zilivyowekwa kwenye sheria.

**Zingatia**: Muda wote, watoa mafunzo waliwakumbusha wanavijiji umuhimu wa vipindi hivi vya mafunzo – kujenga msingi kwa ajili ya uelewa bora wa sheria za utunzaji maliasili na kuwasaidia katika kutengeneza sheria za utunzaji maliasili za vijiji vyao.

Baada ya hatua mbili za mwanzo, wanavijiji (pale hali iliporuhusu) waligawanywa katika makundi na kupewa maswali ya majadiliano ili kupima uelewa wao wa mafunzo. Wakati wa zoezi hili, ambalo lilidumu kwa dakika takribani 30, watoa mafunzo waliyazungukia makundi ya majadiliano ili kuhakikisha kwamba wanavijiji hawatoki nje ya majadiliano. Maafisa kutoka Halmashauri ya wilaya ambao waliongozana na watoa mafunzo walisaidia katika kusimamia mazoezi haya.

### 4.1.3 Hatua ya III:

Baada ya kuweka msingi wa uelewa wa sheria kwa ujumla katika hatua mbili za mwanzo, vipindi vilivyofuata vilihusisha uchambuzi wa sheria mama za maliasili ambazo ziliendana na vijiji. Tena hili lilifanyika kwa nafasi na katika hali iliyohakikisha kwamba wanavijiji wanafuatilia. (Tazama kiambatanisho “A” ya Ripoti hii).

Wanavijiji walipewa kwa ufupi msimamo wa sheria ili kutoa maelekezo katika kuhakikisha kwamba sheria ndogondogo watakazozitunga zinakuwa zinaendana na sheria husika.

Mara nyingi watoa mafunzo walitumia mbinu ya maswali na majibu ili kupata umakini wa wanavijiji. Kwa mfano, wanavijiji waliulizwa kama walikuwa na kanuni zozote zinazohusiana na utunzaji wa maliasili na kanuni zilikuwa zinasemaje. Katika kutoa majibu, watoa mafunzo walisisitiza nafasi ya sheria katika kuonyesha ni kwa kiwango gani kulikuwa na uwiano (au vinginevyo) na sheria.

Vipindi vilifuatiwa na majadiliano katika mfumo wa mazoezi, kama ilivyokuwa katika hatua za I na II.

### 4.1.4 Hatua ya IV:

Hatua hii ilitumika mwishoni na ilihusisha mafunzo kuhusu utengenezaji wa sheria ndogondogo kwa kufuata utaratibu uliowekwa kwenye vifungu husika vya Sheria ya Serikali za Mitaa (Halmashauri za Wilaya) ya mwaka 1982 (kama ilivyobadilishwa).

Watoa mafunzo walikwenda hatua kwa hatua, katika kuweza kujua utaratibu ambao wanavijiji waliutumia katika kutengeneza kanuni ambazo zilikuwepo katika vijiji vingi.

Watoa mafunzo walichukua utaratibu wa kuzipitia kanuni zilizopo kabla ya vipindi na kuzitumia kama mifano katika mafunzo.

Mfano uliotumika pia ulichorwa na ukaachwa kwa kila kijiji. Baada ya watoa mafunzo kukamilisha kipindi hiki, wanavijiji waligawanywa katika makundi na kufanya majadiliano kama ilivyokuwa katika hatua zilizotangulia. (Tazama kiambatanisho “C” kwenye Ripoti hii).

# 5 Ripoti Ya ‘Field’

## 5.1 Kijiji Cha Twasalie (Delta)

| | |
|---|---|
| *Watoa mafunzo:* | Majamba/Mshana |
| *Muda wa mafunzo*: | Siku 3 (Tarehe 3 – 5 Mei 2001) |
| *Wakati/Vipindi*: | Vipindi viwili. Kimoja asubuhi (saa 3.00 asubuhi – 6.00 mchana) na kingine mchana (saa 8.00 – 10.00 jioni) |
| *Idadi ya Wanakijiji:* | Ilitofautiana siku hadi siku lakini wastani wa wanavijiji 38 (Kati yao 7 walikuwa wanawake). |
| *Maafisa wa Wilaya Waliokuwepo*: | Nandi (Idara ya Kilimo), Ndasi (Idara ya Elimu na Utamaduni) na Zuhura (Ofisi ya Maendeleo ya Jamii). |
| *Wengine:* | Rose Hogan (MUMARU) na Heather Hoag (mwanafunzi wa Ph.D kutoka Marekani anayefanya utafiti kuhusu historia ya mazingira ya Mto Rufiji). |

**Siku ya 1:**

Shughuli: Kuchora ramani na uwasilishaji wa mpango wa utunzaji mazingira wa kijiji. Ilionekana kwamba maliasili kubwa ni samaki, madini (chumvi), bidhaa za misitu (ukataji mikoko kwa ajili ya biashara, utengenezaji mitumbwi, ufugaji nyuki) na wanyamapori (mamba, kima, simba, chui, nguruwe pori, ndege na viboko).

**ZINGATIA**: Wanavijiji wamekubaliana kufunga mto Tarachu kwa kipindi cha miezi mitatu ili kuwezesha samaki kuzaliana na kudhibiti shughuli za uvuvi. Wameweka aina fulani ya “sheria” (kanuni) ambazo zililengwa ziwe sheria.

**Siku ya 2:**

Maendeleo ya majadiliano na watoa mafunzo waliwauliza wanavijiji maswali kuweza kutambua matatizo ya mambo ya sheria waliyokumbana nayo katika utekelezaji wa mpango wa utunzaji mazingira wa kijiji.

Iligundulika kwamba kilimo, ukataji mikoko ili kupanda mpunga na wahamiaji wa ukulima kama sababu zilizohusisha matatizo mengine makubwa ambayo yalikuwa na madhara kwenye utunzaji maliasili.

Pia iligundulika kwamba kijiji hiki hakikuwa na aina yoyote ya sheria isipokuwa kuna kanuni za kulinda maliasili. Kanuni zilitengenezwa na kikundi kidogo cha watu (serikali ya Kijiji na wajumbe wa Kamati ya mazingira) ili kutoa mwongozo wa usimamizi wa mazingira na

maliasili katika maeneo waliyokubaliana katika mkutano wa kijiji. Kanuni hizi zimepelekwa katani kwa ajili ya kupitishwa lakini hazikutengenezwa katika mfumo unaokubalika kuzifanya ziwe sheria ndogondogo.

Jambo lingine lililogundulika ni uwepo wa wanyama waharibifu kama nyani, kima, nguruwe pori n.k. Wanakijiji walionekena kutozifahamu sheria zinazowalinda wanyamapori kama sheria ya Uhifadhi Wanyamapori ya mwaka 1974. Wanakijiji pia waliomba watafutiwe soko la nyani na kima.
Pamoja na wanakijiji kusema mto Tarachu umefungwa hakuna hatua zozote za utekelezaji zilizochukuliwa.

Wanakijiji walikuwa wanatumia njia za mila na desturi ili kupambana na wale waliovunja mila za utunzaji maliasili ambazo walisema zilikuwa zinajulikana kwa wanakijiji wengi. Iligundulika, hata hivyo, kwamba wanavijiji wengi hawajui kufungwa mto Tarachu.

Vipindi vya mafunzo vilianza kwa kutumia mfumo ambao umeshaelezwa. Sheria za utunzaji maliasili ambazo mafunzo katika kijiji hiki yalielekezwa zilikuwa:

1. Sheria ya Uvuvi, na Kanuni zilizotengenezwa chini yake.
2. Sheria ya Misitu (pamoja na Sera ya Ufugaji Nyuki).
3. Sheria ya Ardhi Vijijini.
4. Sheria zinazohusiana na ardhi chepechepe.
5. Sheria ya Wanyamapori.
6. Sheria ya Serikali za Mitaa.

**Siku ya 3:**

Marudio kwa ufupi ya siku mbili za kwanza kwa njia ya maswali/majadiliano na kipindi kuhusu utungaji sheria ndogondogo kilianza.

Wanakijiji waligawanywa katika makundi matatu na wakapewa zoezi la majadiliano kuhusu hatua za kufuata katika kutunga sheria ndogondogo.

**Uchambuzi wa Jumla na Mtazamo:**

- Mapengo katika mawasiliano kati ya serikali ya kijiji na wanakijiji yalichangia kwa kiasi fulani katika mfumo uliotumika. Watoa mafunzo walikuwa na tahadhari katika kutoa mazoezi/majadiliano ya vikundi.

- Ili sheria ndogondogo ziweze kufanya kazi vizuri kama inavyotakiwa na serikali kuu ni lazima wananchi wengi wahusishwe katika kuziandaa sheria hizi ndogondogo mwanzoni kabisa. Kama hatua madhubuti hazitachukuliwa na viongozi wa kijiji cha Twasalie kuwajulisha na kuwahusisha idadi kubwa ya wanakijiji katika utengenezaji wa sheria ndogondogo basi hawataziunga mkono kwa mipango yao mizuri na kanuni za usimamizi wa mazingira.

- Uwiano wa kijinsia (mtazamo mbaya wa nafasi ya wanawake katika kijiji) pia ulitiliwa mkazo katika vipindi. Ushiriki wa wanawake (ambao ni washika dau muhimu katika utunzaji wa maliasili za kijiji) katika vipindi ulizuiwa na uwiano mbaya wa kijinsia kijijini. Wakati fulani katika mafunzo, mzee mmoja "alimnyamazisha" mwanamke mmoja ambaye alinyoosha mkono ili kuuliza swali. Alipoombwa kumuheshimu Mwenyekiti, mzee yule alitoka nje huku akivuta wafuasi kadhaa. Kwa kuona hivyo,

mwanamke yule aliamua kutouliza swali lolote, na akasema kwamba atajiuzulu kama mjumbe wa kamati/timu ya maliasili ya kijiji. Watoa mafunzo ilibidi watumie mfumo wa ufundishaji uliozingatia uzoefu huu.

- Ushiriki zaidi wa kidemokrasia ulionekana kwa kuwa kulikuwa na heshima kwa kila mchango uliotolewa na watoa mafunzo.

## 5.2 Kijiji Cha Jaja (Delta)

| | |
|---|---|
| *Watoa mafunzo:* | Kama Twasalie |
| *Muda wa mafunzo*: | Kama Twasalie |
| *Wakati/Vipindi*: | Vipindi viwili vya mafunzo. Kimoja asubuhi (saa 3.00 asubuhi – 6.00 mchana) na kingine mchana (saa 8.00 – 10.00 jioni) |
| *Idadi ya Wanakijiji:* | 42 (wanawake 11) |
| *Idadi ya siku:* | Siku 3 (Tarehe 7 – 9 Mei, 2001) |

**Siku ya 1:**
Kuchora ramani ya kijiji na uwasilishaji wa mpango wa utunzaji mazingira wa kijiji. Watoa mafunzo pia waliitambua mipaka ya kijiji na maliasili zinazopatikana kijijini.

Aina kuu za maliasili zinazopatikana ni samaki, ndege, kamba, mashamba ya mpunga(lakini eneo hili lipo nje ya kijiji), bidhaa za misitu (ufugaji nyuki na mikoko) na madini (chumvi).

Wanakijiji walijali zaidi shughuli ambazo waliziona zinaharibu maliasili ikiwa ni pamoja na ukataji miti ya kutengenezea mitumbwi na majahazi ya kusafirisha mikoko kwenda Zanzibar na Mafia na uvuvi haramu wa kamba kwa kutumia meli kubwa baharini. Mengine yalikuwa ni matatizo yaliyotokana na wanyama waharibifu na ugumu unaowakabili skauti wa kijiji katika kuwakamata na kushughulika na watu wanaovunja kanuni zilizopitishwa na kijiji.

Pia shida ya mifugo kutembea holela kwenye mashamba na kula mbogamboga zenye vitamini A kwa wingi kutoka bustani za wanawake ilionekana kuwa tatizo sugu.

**Siku ya 2:**
Majadiliano ya jumla, vipindi vya maswali na majibu vilitolewa na watoa mafunzo kama njia ya kukumbusha yaliyofundishwa jana ili kuchochea masuala yanayosumbua ya sheria na kuweka msingi wa aina ya sheria watakazowafundisha wanakijiji.

Matatizo mengine yalitambuliwa kama umiliki wa ardhi ambamo maliasili zinapatikana na utekelezaji wa sheria ndogondogo kwa kuwatumia skauti wa kijiji.

Sheria husika na zinazotumika ambazo zilifundishwa katika kijiji hiki na kujadiliwa siku hii ni pamoja na Sheria ya Uvuvi, Sheria ya Ardhi Vijijini, Sheria za Mifugo na Kilimo, Sheria ya Misitu na Sheria ya Serikali za Mitaa.

**Siku ya 3:**
Majumuisho ya siku mbili za mwanzo na kujibu maswali.

Halafu, hatua za kufuata katika utengenezaji wa sheria ndogondogo za maliasili zilibainishwa.

Watoa mafunzo waliwagawanya wanakijiji katika makundi na kujadili mambo yaliyofundishwa katika vipindi kwa njia inayofanana na mahakama. Ni wanakijiji peke yao walishiriki na watoa mafunzo walikaa na kufanya utafiti wa uelewa wao wa vipindi.

**Uchambuzi wa Jumla na Mtazamo:**
Kwa wastani, ushiriki na uelewa wa wanakijiji ulikuwa mzuri. Asilimia kama 70 hivi ya wanakijiji walionekana kuelewa yaliyofundishwa na kuwaongezea ufahamu.

Ilionekana wazi kwamba uwepo wa meli kubwa za uvuvi wa kamba karibu na pwani ni tatizo kubwa hasa kwa uvuvi unaofanyika eneo la karibu na pwani ambalo kwa mujibu wa sheria ya uvuvi ni marufuku kuvua.

Kwa wanakijiji kuyaelewa mafunzo vyema ni uthibitisho wa nafasi muhimu kama ilivyoonyeshwa kwa washiriki wote ilionyesha kwamba wamefikia kiwango cha juu cha uelewa wa mambo ya kisheria yenye kuhusika na maliasili zao.Utengenezaji wa sheria ndogondogo ulioonyeshwa na wanakijiji unatia moyo. Uwezo wa serikali ya kijiji na kamati ya mazingira ya Kijiji kwa kiasi fulani ni wa juu lakini ilionekana kwamba kundi hili muhimu linahitaji kuwashirikisha wanakijiji wengi na kupata uungwaji mkono wa sheria ndogondogo wanazozipendekeza

## 5.3 Kijiji Cha Mtanza Msona

| | |
|---|---|
| *Watoa mafunzo:* | Majamba/Macha |
| *Maafisa wa Wilaya:* | |
| *Waliokuwepo*: | Kilonzo (Misitu), Ohii (Afisa Wanayamapori), Mwambeso (Kilimo) |
| *Muda wa mafunzo*: | Siku 3 (Tarehe 13 – 15 Mei 2001) |
| *Muda/Vipindi*: | Vipindi viwili. Asubuhi na Mchana (saa 4.00 asubuhi – 6.00 mchana) na kingine mchana (saa 8.00 – 9.00 alasiri) |
| *Idadi ya Wanakijiji:* | Wastani wa wanakijiji 42 (wanawake 13). |
| *Wengine:* | Rose Hogan (MUMARU) |

**Siku ya 1:**
Wanakijiji walichora ramani ya kijiji na wakaonyesha aina kuu za maliasili zilizopo kijijini. Uwasilishaji na majadiliano ya mpango wa utunzaji mazingira wa kijiji ulifanyika. Watoa mafunzo waliona kwa uhalisi utunzaji wa maliasili, matatizo husika ya kisheria na vikwazo vinavyokikabili kijiji.

**Maliasili kuu zilizoonekana ni:**
- Bidhaa za misitu (ukataji haramu wa miti na ufugaji nyuki).
- Samaki (wanaotokana na maziwa, mabwawa na mito).
- Ardhi chepechepe; na
- Wanyamapori (kima, simba n.k. Kijiji kinapakana na Pori la Wanyamapori la Selous) na wanakijiji wangependa kuwa na eneo la usimamizi wa wanyamapori la kijiji.
- Kuna maeneo yanayopimwa kwa uchimbajij mafuta Kaskazini Magharibi mwa kijiji.
- Kuna mkataba wa kambi ya watalii unaomuhusisha mwekezaji mmoja na kijiji kinapendelea kuwepo kwa mradi wa utalii wa wanakijiji.

**Siku ya 2:**
Watoa mafunzo walijadili pamoja na wanakijiji matatizo wanayopambana nayo katika utunzaji wa maliasili. Wanakijiji waliwajulisha watoa mafunzo kwamba kulikuwa na mgogoro unaofukuta kati ya kijiji na utawala wa Pori la Wanyamapori la Selous kuhusu mipaka ya kijiji na Pori la Selous. Wanakijiji walidai kwamba mipaka ya Selous "imerekebishwa" na katika kufanya hivyo wakaingia sehemu ya ardhi ya kijiji.

Serikali ya kijiji imeweka aina fulani ya sheria za kusimamia na kudhibiti matumizi ya maliasili zinazopatikana kijijini. Watoa mafunzo walipata fursa ya kuzipitia sheria hizi.

Mafunzo yalianza siku ya pili kwa kutoa utangulizi wa sheria, ukifuatiwa na upitiaji wa sheria zinazohusiana na utunzaji wanyamapori na uvuvi.

**Siku ya 3:**
Watoa mafunzo walitoa majumuisho ya siku iliyotangulia kwa njia ya maswali na majibu. Mafunzo yaliendelea kwa kuangalia vifungu vya Sheria ya Ardhi Vijijini (kwa kuzingatia mgogoro uliopo kati ya kijiji na Pori la Akiba la Wanyamapori la Selous), msisitizo uliwekwa kwenye uwekaji wa mipaka ya kijiji na usajili wa ardhi ya kijiji. Sheria kuhusu misitu na ufugaji nyuki pamoja na sera husika ziliangaliwa.

Kuhusu ardhi iliyotolewa kwa mwekezaji wa kambi ya watalii watoa mafunzo waliwashauri wanakijiji kwamba kijiji kina mamlaka kuhusu ardhi yake na kwamba sio wilaya wala serikali kuu yenye mamlaka ya kugawa ardhi ya kijiji kwa watu wengine kama wanakijiji hawataki. Walishauri kwamba wanakijiji wapate maelezo ya kina ya mwekezaji na eneo husika lipimwe na kuona kama ni eneo la kijiji au la halafu wachukue hatua zipasazo.

Mafunzo kwenye vifungu husika vya Sheria ya Serikali za Mitaa na baadaye utaratibu wa kutengeneza sheria ndogondogo za utunzaji wa maliasili pia ulifundishwa.

Wanakijiji waligawanywa kwenye makundi matatu na kupewa mazoezi na baadaye yakafanyika majadiliano yakiongozwa na watoa mafunzo.

**Uchambuzi wa Jumla na Mtazamo:**
Wanakijiji walikuwa tayari na walikuwa na hamu ya kutekeleza mipango ya maendeleo ili kudhibiti matumizi ya maliasili zilizopo kijijini.

Wanakijiji walisema wanakatishwa tamaa kwamba Halmashauri ya Wilaya haitambui jitihada zao katika utunzaji wa maliasili. Kwa mfano, walisema kwamba waliwakamata watu waliokuwa wanakata miti,wanapasua mbao na wakawakabidhi kwa mamlaka zinazohusika lakini jitihada zao hazijatambuliwa. Hili linavunja moyo wa uhifadhi maliasili na linaweza kufuta kabisa nia na madhumuni ya mafunzo. Pia suala hili lilijitokeza katika kijiji cha Mbunju Mvuleni.

Wanawake walishiriki kikamilifu katika kijiji hiki ukilinganisha na vijiji vyote ambavyo mafunzo yalifanyika. Kuna mwanamke ambaye ni makamu Mwenyekiti wa Kamati ya maliasili ya kijiji na wawili ambao wamepata mafunzo ya uskauti wa kijiji.

Kwa wastani asilimia 60 ya wanakijiji ambao walihudhuria mafunzo walielewa mambo muhimu.

## 5.4 Kiji Cha Mbunju Mvuleni Na Vitongoji Vya Mpima na Mupi

| | |
|---|---|
| *Watoa mafunzo:* | Majamba/Macha |
| *Waliokuwepo*: | Mwambeso (Kilimo), Bainga (Kilimo), Sagara (Uvuvi) na John (Afisa Wanyamapori wa Wilaya). |
| *Wengine:* | Rose Hogan (MUMARU) na Edmund Barrow (IUCN). |
| *Muda wa mafunzo*: | Siku 3 (Tarehe 17 – 19 Mei 2001) |
| *Muda/Vipindi*: | Vipindi viwili. Asubuhi na Mchana (saa 4.00 asubuhi – 7.00 mchana) na kingine mchana (saa 8.00 – 9.00 alasiri) |
| *Idadi ya Wanakijiji:* | Wanakijiji 45 (wanawake 15). |

**Mtazamo wa Awali:**
Kulikuwa na mgogoro kati ya wanakijiji. Baadhi ya wanakijiji walikuwa wanachukuliwa kama "waliotengwa" au hasa "wavamizi" wa ardhi ya kijiji, kwa kuandikishwa vijiji vingine lakini wakiwa wanatumia maliasili za kijiji kingine. Wanakijiji kutoka Mupi na wale wa kutoka Mpima walijisikia kwamba wanachukuliwa kama "wavamizi".

Mgogoro huu mwanzoni ulifanya kazi ya watoa mafunzo kuwa ngumu lakini Rose Hogan aliweza kupunguza jazba za wanakijiji katika hatua za mwanzo. Ingawaje msuguano uliendelea kujitokeza, watoa mafunzo waliweza kuuondoa kila ulipojitokeza. Kwa kiasi kikubwa hili liliathiri vipindi vya mafunzo kwa kuwa watoa mafunzo mara kwa mara walikuwa wanaombwa kuelezea mambo ambayo yalilenga kwenye mgogoro wakati wa vipindi vya maswali na majibu.

**Siku ya 1:**
Wanakijiji kutoka Mupi na Mpima ilibidi wasafirishwe na gari moja kutoka na kwenda eneo la mafunzo (Mbunju) kwa sababu ya umbali. Kwa hali hiyo vipindi vilichelewa na vilikuwa vifupi ukilinganisha na vijiji vingine. Hali hii pamoja na mgogoro, ulifanya vipindi vya mafunzo viwe vigumu lakini watoa mafunzo waliweza kukabiliana na hali hiyo.

Ramani ya kijiji ilichorwa na mpango wa usimamizi wa mazingira wa kijiji uliwasilishwa na wanakijiji wa Mbunju Mvuleni na kujadiliwa licha ya mgogoro na dalili za kutokubaliana kutoka kwa wanakijiji kutoka vitongoji vya Mupi na Mpima. Watoa mafunzo waliweza kutambua maliasili muhimu na juhudi zilizochukuliwa kuzihifadhi.

Maliasili muhimu katika kijiji zilitambuliwa kwamba ni wanyamapori (tembo,nyati, simba, kima, mamba, viboko na aina mbalimbali za ndege), bidhaa za misitu (ufugaji nyuki na ukataji miti) na bidhaa za samaki. Shughuli nyingine pekee iliyoweza kuonekana kwamba ina uwiano na utunzaji maliasili ilikuwa ni kilimo (umwagiliaji) katika eneo la Segeni.

**Siku ya 2:**
Ilikuwa ni siku ya Ijumaa na mafunzo ilibidi yarekebishwe ili kuwapa fursa Waislamu kwenda msikitini kusali. Watoa mafunzo ilibidi wachukue tahadhari kwa suala hili na mfumo wa ufundishaji ilibidi utengenezwe upya. Vipindi vilikuwa vifupi huku maswali machache yakiruhusiwa.

Kipindi kilianza kwa muhtasari wa sheria kwa ujumla na kuzipitia sheria za wanyamapori, uvuvi na misitu.

**Siku ya 3:**
Siku ilianza kwa upitiaji wa haraka wa kipindi cha siku iliyopita na kisha kikafuatia kipindi cha kujadili Sheria ya Ardhi Vijijini, vifungu husika vya Sheria ya Serikali za Mitaa na utaratibu na hatua za kufuata katika kutengeneza sheria ndogondogo za utunzaji maliasili.

Baada ya kupunguza jazba miongoni mwa wanakijiji kwa kiasi fulani, watoa mafunzo walitoa zoezi baada ya kuwagawanya wanakijiji katika makundi. Wanakijiji walifanya majadiliano na kuwasilisha walichoona mbele ya wote.

**Uchambuzi wa Jumla na Mtazamo:**
Kwa wastani asilimia 50 ya wanakijiji waliyaelewa mafunzo. Mwanamke mmoja ni skauti na inaonekana anaheshimiwa na wanakijiji wenzake.

Kwa sababu ya mgogoro uliojadiliwa hapo juu, vipindi vya mafunzo kwa kiasi fulani vilikosa ushirikiano kutoka kwa wanakijiji kwa sababu maswali mengi yalikuwa yanaelekezwa katika kujaribu kupata kutoka kwa watoa mafunzo kwamba nani alikuwa na haki gani.

Watoa mafunzo walipendekeza kwamba ili kutatua migogoro ya umiliki wa ardhi kijijini ni lazima kuwe na kamati ya ardhi ya kijiji itakayokuwa mshauri Mkuu wa Serikali ya Kijiji katika ugawaji wa ardhi Kijijini na migongano iliyopo itatuliwe katika ngazi ya kijiji na kama itashindikana kabisa basi anayehisi hajaridhika aende mahakamani kutafuta haki yake.

Kwenda Mahakamani, inasisitizwa, iwe ni njia ya mwisho kabisa ili kukuza maelewano mazuri kati ya wanakijiji.

# 6 Ufupisho wa Mafunzo kwa Ujumla

- MUMARU wamefanya kazi kubwa katika kuwapatia wanakijiji uwezo muhimu katika kutunza maliasili. Uelewa wa wanavijiji katika kozi za mafunzo ulifanya kazi ya watoa mafunzo kuwa rahisi kidogo.

- Lengo la mafunzo lilikuwa kwa kiasi kikubwa limefikiwa. Uelewa wa wanavijiji kuhusu mambo ya msingi ya sheria za maliasili kwa kiasi fulani ulipanuliwa. Kwa ujumla kiasi cha watu 200 (pamoja na Maafisa wa Wilaya) walioongozana na watoa mafunzo walifaidika.

- Kunaweza kuwa na haja ya kufanya uchambuzi (ufuatiliaji) wa kuonyesha ni kwa kiasi gani kundi la walengwa linamudu katika kutumia sheria katika kutunza na kusimamia maliasili.

- Ziara za mara kwa mara za maafisa na Wilaya zinaweza kusaidia katika hili.

- Jitihada zaidi zinahitajika kuweza kuwahamasisha wanavijiji kuondokana na vikwazo vya kiutamaduni na kijamii ili kuwashirikisha washikadau wote katika utunzaji wa maliasili za vijiji na kuwafundisha njia mbalimbali za kuwasiliana na wanakijiji wote.

- Pia ni muhimu kuwapa wanavijiji ujuzi wa usimamizi na utawala kwa ujumla kwa njia za kidemokrasia na uwazi.

# 7 Viambatanisho

## 7.1 Kiambatanisho 'A'

**Muhtasari wa Sheria Zinazohusiana na Utunzaji Maliasili Silisofundishwa Vijijini**

**Sheria Ya Uvuvi Ya Mwaka 1970**
Sheria hii inazungumzia ulinzi, uhifadhi, maendeleo, usimamizi na udhibiti wa samaki, bidhaa/mazao yatokanayo na samaki, uoto wa chini ya bahari na mazao yake, na mambo mengineyo yanayohusiana nayo.

Sheria hii inampa mamlaka Rais kumteua Afisa Mkuu wa Uvuvi na Waziri anayeshughulika na uvuvi amepewa mamlaka ya kuwateua maafisa uvuvi na pia kutunga sheria ndogo ndogo zinazohusiana na uvuvi.

Pia Waziri ana mamlaka ya kutangaza eneo lolote kwamba limefungwa kwa shughuli za uvuvi na atakayekiuka agizo hilo la Waziri ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria.

Waziri alitunga sheria ndogondogo mwaka 1973 zikitoa maelezo, pamoja na mengine, kwamba ni marufuku kwa nyavu za uvuvi kuwa ndogo zaidi ya inchi mbili na nusu na vyombo vyote vya uvuvi lazima visajiliwe na Wizara ya uvuvi. Ni marufuku kuvua samaki kwa kutumia vyombo vikubwa vya uvuvi yaani meli za uvuvi bila kibali.

Meli kubwa za uvuvi haziruhusiwi kuvua samaki maili kumi na mbili kutoka pwani ya bahari. Atakayefanya hivyo ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria hii.

Vyombo vitakavyotumika wakati wa kufanya makosa chini ya sheria hii vitataifishwa na kuwa mali ya taifa.

**Sheria Ya Wanyamapori Ya Mwaka 1974**
Sheria hii inazungumzia ulinzi, uhifadhi, maendeleo, usimamizi na udhibiti wa wanyamapori na mazao yatokanayo na wanyama na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Sheria hii inampa mamlaka Rais kumteua Mkurugenzi wa Wanyamapori ambaye atakuwa na mamlaka na wajibu wa utawala bora wa maafisa wengine.

Mkurugenzi wa wanyamapori amepewa mamlaka ya kuwateua maafisa wanyamapori watakaomsaidia kutekeleza sheria hii ya wanyamapori na sera za wanyamapori za mwaka 1998.

Chini ya sheria hii Rais amepewa mamlaka ya kutangaza eneo lolote la nchi kuwa hifadhi ya wanyamapori na Waziri ana mamlaka ya kutangaza eneo lolote la nchi kuwa eneo la udhibiti wa wanyamapori. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuwinda katika maeneo haya yaani hifadhi ya wanyamapori au eneo la udhibiti wa wanyamapori bila kupata kibali cha Mkurugenzi wa Wanyamapori na atakayekiuka atachukuliwa hatua za kisheria. Pia ni marufuku kuchoma moto, kukata miti, kukamata au kuua wanyamapori pamoja na kulima katika maeneo ya hifadhi.

Waziri pia ana mamlaka ya kutangaza kwamba aina fulani ya mnyama au wanyama kuwa ni Mnyama wa Taifa na ni marufuku mtu yeyote kuwinda, kuua, kukamata au kujeruhi mnyama ambaye ametangazwa kuwa mnyama wa Taifa bila kibali cha Mkurugenzi wa Wanyamapori.
Sheria hii pia inazungumzia uwindaji, ukamataji na upigaji picha Wanyamapori. Uwindaji hauruhusiwi bila kibali. Pia ni marufuku kukamata mnyamapori bila kibali. Sheria vilevile inakataza kuwinda au kuua mnyama mwenye mimba au mwenye watoto au watoto wenyewe.

Mnyama anayeuawa kwa ajali au makosa ni lazima yule aliyemuua amchune ngozi, atoe pembe, meno au nyara ya thamani na atoe ripoti kwa Afisa Wanyamapori aliye karibu.

Sheria hii inaruhusu, ingawa kwa masharti, mtu kumuua mnyama ili kulinda maisha yake au mali yake. Masharti ni kwamba mnyama huyo asiwe amechokozwa au mtu huyo asiwe anafanya kosa ndani ya sheria hii wakati wa kumuua mnyama huyo.

Sheria hii pia inatoa adhabu mbalimbali kwa makosa chini ya sheria hii. Vilevile sheria hii ina orodha za wanyamapori, ndege pamoja na wanyama hatari.

**Sheria Ya Misitu Ya Mwaka 1959**
Sheria hii inazungumzia uhifadhi na utunzaji wa misitu na mazao yatokanayo na misitu.

Mhifadhi Mkuu wa Misitu na maafisa misitu pamoja na wafanyakazi wa idara ya misitu ndio wanaowajibika katika utekelezaji wa sheria hii.

Waziri ana mamlaka ya kutangaza eneo lolote kuwa hifadhi ya misitu au hifadhi ya misitu ya serikali ya mtaa. Ni marufuku kuchukua bidhaa/mazao yoyote ya misitu bila kibali cha Mhifadhi Mkuu wa Misitu.

Msitu wa hifadhi wa serikali ya mtaa utatunzwa na serikali ya mtaa husika ambayo ina uwezo wa kumteua meneja wa msitu huo. Mhifadhi Mkuu wa Misitu ndiye atakuwa mshauri mkuu wa utunzaji wa msitu wa hifadhi wa serikali ya mtaa.

Ni marufuku kukata miti, kuchoma moto, kulima, kuishi, kujenga, kuchunga mifugo, kurina asali n.k. katika msitu wa hifadhi. Ni wajibu wa jamii nzima kusaidia utunzaji wa misitu ya hifadhi dhidi ya uharibifu wa aina yoyote ile.

Waziri ana mamlaka ya kutangaza aina fulani za miti kuwa ya hifadhi hata kama haipo kwenye msitu wa hifadhi na mtu yeyote atakayekata mti/miti hiyo bila kibali atachukuliwa hatua za kisheria.

Vibali katika sheria hii hutolewa na Mhifadhi Mkuu wa Misitu au mtu yeyote aliyeruhusiwa naye. Pia wana mamlaka ya kufuta kibali chochote wakati wowote kama aliyepewa kibali hicho atakiuka masharti yaliyomo kwenye kibali.

Sheria hii pia inatoa adhabu kwa yeyote atakayekiuka masharti ya sheria hii.

**Sheria Ya Ardhi Vijijini Ya Mwaka 1999**
Sheria hii inazungumzia usimamizi na utawala wa ardhi katika vijiji na mambo yanayohusiana na hayo.

Mojawapo ya kanuni kuu za sera ya Taifa ya Ardhi kama zilivyoainishwa ndani ya sheria hii ni kuhakikisha kwamba ardhi inatumika vizuri na matumizi hayo yanaendana na kanuni za maendeleo endelevu.

Kanuni nyingine kuu ni kwamba wanawake wana haki sawa na wanaume kumiliki ardhi.

Sheria hii inatamka kwamba kuna aina kuu nne za ardhi nchini Tanzania nazo ni ardhi ya jumla; ardhi ya umma; ardhi ya vijiji; na ardhi ya hifadhi. Ardhi ya vijiji ndiyo inasimamiwa na sheria hii.

Mamlaka ya usimamizi wa ardhi ya kijiji yamewekwa mikononi mwa serikali ya kijiji kama mdhamini wa wanakijiji. Katika usimamizi wa ardhi ya kijiji, serikali ya kijiji ni lazima

izingatie kanuni ya maendeleo endelevu na uhusiano kati ya matumizi ya ardhi, maliasili nyinginezo na mazingira ya kijiji na ardhi ya kijiji.

Serikali ya kijiji ndio yenye mamlaka ya ugawaji ardhi kijijini na ni lazima ipate idhini ya Mkutano Mkuu wa kijiji kabla ya kugawa ardhi yoyote ya kijiji. Pia serikali ya kijiji ina uwezo wa kuunda kamati ya ardhi ya kijiji ambayo itakuwa inatoa ushauri kuhusu usimamizi wa ardhi ya kijiji. Kamati hii itakuwa na wajumbe 7 na watatu (3) ni lazima wawe wanawake.

Kamishna wa ardhi na Halmashauri ya wilaya watakuwa ni washauri wa serikali ya kijiji kuhusu matumizi ya ardhi.

Mtu ambaye si mwanakijiji anaweza kumiliki ardhi kijijini iwapo serikali ya kijiji itapata idhini ya mkutano mkuu wa kijiji kumgawia mtu huyo ardhi kijijini.

Ikiwa kuna migogoro ya ardhi kijijini basi Baraza la Ardhi kijijini litakuwa na mamlaka ya kusuluhisha na ikishindwa kutoa usuluhisho basi shauri hilo litapelekwa mahakamani.

## 7.2 Kiambatanisho ‘B’

### Mahudhurio Ya Mafunzo Ya Sheria: Kijiji Cha Mtanza Msona

| JINA | WADHIFA |
|---|---|
| | |
| JUMA AMIRI KOPA | Scout wa Mazingira |
| BAKARI H. WAMBANGURU | Mkulima |
| YUSUFU AMIRI NYAMUNGUMI | Mjumbe S/Kijiji |
| MUSSA S. MPITU | Mkulima |
| ARUFANI ATHUMANI MAZELA | M/kiti wa Kijiji |
| ISMAIL SAID LUSONZO | Mwenyekiti K/Mazingira |
| SIKUDHANI M. MGANE | Mafunzo - Nyuki |
| SEFU S. LUHANDO | Katibu - Mazingira |
| RAMADHANI A. MGOMBELWA | Mjumbe K/Mazingira |
| IDDI S. NDUMBO | - “ - |
| BAKARI ABEDI | - “ - |
| SALUMU K. KILANGATI | - “ - |
| HASSANI M. MPONDELA | Mjumbe S/Kijiji |
| FALE A. MBJONDE | Mafunzo Mazao Miti |
| MOSHI A. MAKASAMALA | M/K/Mazingira |
| BAKARI M. MBONDE | M/S/Kijiji |
| ABDALLAH MGANE | Mkulima |
| KHADIJA OMARI MWEGERO | M/K/Mazingira |
| ZANDA MILANDU | M/S/Kijiji |
| IMANI A. MILANDU | M/S/Kijiji |
| FATUMA A. MBONDE | M/S/Kijiji |
| AVITAKA I. MILANDU | Mkulima |
| ROSE HOGAN | MSHAURI/MUMARU |
| MOHAMED M. PUNGAHEWA | VEO |
| HASSARA H. MANGITA | Mkulima |
| ABDALLAH S SELELANI | Mkulima |
| BIBIYE MWALIMU | Mkulima |
| SALUMU H. WINGI | Mkulima |
| PILI H. MKUNDUGE | Mafunzo Nyuki |
| SHABANI MZAMILU | M/K/Mazingira |
| KURWA A. MBONDE | Mjumbe Kamati ya Mazingira |
| SAID S. NDULI | Mjumbe Kamati ya Mazingira |
| TWAKEE J. SAMATA | Makamu M/Kiti Mazingira |

| | |
|---|---|
| ALLY SEIF MBITEHENI | Mkulima |
| MOSHI M. NDULI | Scout Mazingira |
| KISIA A. MKINGA | Mjumbe Kamati Mazingira |
| SHABANI S. NYANGALIO | Mweka Hazina K. Mazingira |
| MOSHIU. HAFUMA | Scout Mazingira |
| MKE JINA M. MBONDE | Mkulima |
| TABU NDETE | Mkulima |
| KAWANIA H. SELELANI | Mkulima |
| MOHAMEDI NGONDO | Mjumbe Serikali ya Kijiji |
| FAIDA MBONDE | Mjumbe Kamati ya Mazingira |
| FIKIRA MWEGERO | Mkulima |
| HUSSEIN HARRY | Idara ya Kilimo |
| PHILIPO KILONZO | Idara ya Misitu |
| JUMA MKUNGURA | Afisa Wanyama Maripo |
| P.A. MWAMBESO | Idara ya Kilimo |
| T.M. MACHA | LEAT |
| DR. MAJAMBA | LEAT |
| SALIMU M. PINGI | Mjumbe S/Kijiji |
| ABDALLAH H. NZILAIMO | Mwenyekiti wa Kitongoji |
| MUSSA A. MTOU | M/S/Kijiji |
| HAMISI A. MILANDU | Mkulima/Mwanakijiji |
| ALLY MGONZA | Mjumbe K/Mazingira |
| MOHAMED MTANGE | Mkulima |
| BIBIYE R. MOTA | Mjumbe S. Kijiji |
| ALLY SHAMTE MGONZA | Mkulima |
| NIACHIENI S. WAMBANGURU | Scout Mazingira |
| JUMANNE UZINDU | Mwanamaigizo |
| KILANGATI KISOMA | Mkulima |
| HERI H. NGWINYE | Scout Mazingira |
| HAMISI WAMBANGURU | Mwanakijiji |
| MUSSA MPITU | Mjumbe S. Kijiji |
| ALLY MCHAWI | Mkulima |
| RAMADHANI MILANDU | Mkulima |
| IDDY MMANYEMA | Mjumbe Kamati Mazingira |
| MOSHI MANGORWA | Mjumbe Kamati Mazingira |
| SALUMU MTANGE | Mkulima |
| ABDRAMANI NDULI | Mkulima |
| SAIDI MILANDU | Mwenyekiti wa Kitongoji |
| DIFA S. NGARANDA | Mkulima |
| RASHIDI I. MPITU | Mkulima |
| NIACHIENI YUMBA | Scout Mazingira |
| JUMA NINDI | Mwanakijiji |

**Mahudhurio ya Mafunzo ya Sheria: Kijiji Cha Mbunju Mvuleni.**

| | | |
|---|---|---|
| HAMISI ALLY NKWANYWE | - | Mbunju/Mvuleni |
| MOSHI ALLY MLANZI | - | Mbunju/Mvuleni |
| HAMISI S. MLAWA | - | Mbunju Mvuleni |
| YUSUFUH. MATIMBWA | - | Mbunju Mvuleni |
| JUMA O. NGULANGWA | - | Mbunju/Mvuleni |
| MAJURID A. MKWANYWE | - | Mbunju/Mvuleni |
| ATHUMANI M. MKUMBA | - | Mbunju/Mvuleni |
| MBWANA S. NJICHO | - | Mbunju/Mvuleni |
| RAJABU S. MLANZI | - | Mbunju/Mvuleni |
| SALUMU S. MATIMBWA | - | Mbunju/Mvuleni |
| RAMADHANI A. MKOMBWA | - | Mbunju.Mvuleni |
| HASHIMU S. MHENGA | - | Mbunju/Mwenyekiti Kijiji |
| HATIBU A. MLANZI | - | Mbunju/Mvuleni |
| JUMA S. MTAMBO | - | Mbunju/Mvuleni |
| HAMISI S. MKIMA | - | Mpima |
| HADIJA S. MKWANYWE | - | Mpima |
| KHADIJA S. NGINDO | - | Mpima |
| SHUKURU S.MTAMBO | - | Mpima |
| SHABANI NYUMBA | - | Mpima |
| ABDALAH MKOBMWA | - | Mpima |
| ABDALLAH MTINGE | - | Mpima |
| KASIMU A. NGWERE | - | Mpima |
| OMARI NDEMBO | - | Mupi |
| SHUKURU O. MATIMBWA | - | Mvuleni |
| ASIA M. MKOPA | - | Mvuleni |
| MWADHANI R. NGUBEGE | - | Mvuleni |
| SULTANI M. MAKASALA | - | Mvuleni (VEO) |
| HASHIMU A. NGEMBA | - | Mupi |
| SEIF OMARY NGWERE | - | Mpima |
| ADRAMANI Y. MTETA | - | Mpima |
| HABIBA OMARY MNIWA | - | Mpima |
| SOFIA OMARY MAPANDE | - | Mupi |
| JARARA J. MBOTONI | - | Mpima |
| TULIA M. NGWERE | - | Mpima |
| MWAJUMA R. NJIWA | - | Mpima |
| ASHA ISSA ALIMASI | - | Mupi |
| MWANAIDI M. MKIU | - | Mupi |
| IMANI ISSA ALMASI | - | Mupi |
| ZAINABU K. KWANGAYA | - | Mupi |
| MWAJUMA S. MTINGE | - | Mupi |
| KESI KITUMBI | - | Mpima |
| SAIDI A. LILENDE | - | Mpima |
| JUMANNE S. MPOMBO | - | Mupi |
| HAJI S. NGEMBA | - | Mupi |
| ABDALLAH KASIMU | - | Mbunju/Mvuleni |
| SIASA H. MATIMBWA | - | Mbunju/Mvuleni |
| MOSHI A. NGAPULA | - | Mbunju/Mvuleni |
| HAMISI A. CHAMPINGO | - | Mbunju/Mvuleni |
| SALUMU MKUMBA (KABOKO) | - | Mvuleni |
| RAMADHANI RADA | - | Mvuleni |

| | | |
|---|---|---|
| MOSHI SAIDI MAHILO | - | Mvuleni |
| MAUA IPUMU | - | Mvuleni |
| HAKI MACHUNGU | - | Mvuleni |
| E. JOHN | - | Afisa Wanyamapori (W) |
| BAINGA I.B. | - | Idara ya Kilimo |
| SAGARA | - | Idara ya Samaki(Maliasili) |
| P.A. MWAMBESO | - | Idara ya Kilimo |
| MACHA T. | - | LEAT |
| DR. MAJAMBA | - | LEAT |
| ROSE HOGAN | | Mshauri Maendeleo Jamii MUMARU |

**Mahudhurio ya Mafunzo ya Sheria: Kijiji Cha Tawasalie**

| NAME | | WADHIFA |
|---|---|---|
| RAJAB MUBA | - | Mwenyekiti S/Kijiji |
| AMIRI. KITANDA | - | Mjumbe Kamati ya Mazingira |
| MWAJUMA M. BARUANI | - | Mjumbe Serikali ya Kijiji |
| ASHURA AMIRI HAME | - | Mwanakikundi Matunda |
| MARIAMU HUSSEIN | - | Mwanakikundi Matunda |
| MRISHO BURUANI | - | Mwanakijiji |
| REMA URONGO | - | Mwanakijiji |
| MAULID SHABANI | - | Kamati ya Mazingira |
| SALIMA SALAMALA | - | Mjumbe Kamati ya Mazingira |
| MAIMUNA HAMIS NDEZI | - | Mwanakijiji |
| MAISHA SHABAN | - | Mjumbe Kamati ya Mazingira |
| LAMLA HAMIS NDEZI | - | Mjumbe Serikali ya Kijiji |
| YUSUF M. GOYA | - | Mwanakijiji |
| SHWARI JUMANNE KITANDA | - | Mwanakikundi -Korosho |
| SHABANI SULTANI | - | Mjumbe Kamati ya Mazingira |
| ABDURAHAMAN SHABANI | - | Mjumbe Kamati ya Mazingira |
| MOHAMED MIKAVU | - | Mjumbe Kamati ya Mazingira |
| JUMA ISSA MONERO | - | Kikundi cha Nyuki |
| JUMANNE J. NDONGORO | - | Kikundi cha Matunda |
| BAKARI IDDI KISOMA | - | Mwenyekiti Kamati/Mazingira |
| JAMADI HAMISI | - | Skauti |
| MOHAMEDI KASSIM | - | Skauti |
| SHABANI MCHENGA | - | Kikundi cha Nyuki |
| RAMADHANI MUHENGA | - | Mwanakijiji |
| MOHAMEDI BONGO | - | Kikundi cha Nyuki |
| JUMA AMANI NJOWE | - | Mwanakijiji |
| MUHSINI MBENDA | - | Mwanakijiji |
| MOHAMEDI SHAHA | - | Mwanakijiji |
| MIKIDADIJ Y. GOYO | - | Shehe wa Kijiji |
| SAIDI M. SALAMALA | - | Mwanakijiji |
| SELEMANI PONGWA | - | Skauti |
| RASHIDI GOYO | - | Mwl. dini |
| JUMANNE RITOKI | - | Mwanakijiji |
| MIRAJI J. MWINGO | - | Katibu Kamati ya Mazingira |
| SHABANI H. KOGE | - | Afisa Mtendaji Kijiji |
| ABDURAHAMANI SHAHA | - | Mjumbe Serikali ya Kijiji |
| HASANI ISSA MONERO | - | Mwanakijiji |
| KASSIM H. NDEZI | - | Mjumbe Serikali ya Kijiji |
| RAJABU H. ROMBEROMBE | - | Mjumbe Serikali ya Kijiji |
| HAMISI MMEYA | - | Mwanakijiji |
| OMARI MALIKI | - | Mwanakijiji |
| ALLY SULTANI NDEZI | - | Mwanakijiji |
| SHABANI H. MIROKA | - | Mwanakijiji |
| SHABANI NDEKYO | - | Kikundi cha Nyuki |
| MWAJUMA ISSA | - | Mwanakijiji |
| MWEMA MWINYIKONDO | - | Mwanakijiji |
| BASHIRU HAMISI | - | Mwanakijiji |
| AMIDA MOHAMED | - | Kikundi cha Mboga na Matunda |
| SHABANI MOHAMED | - | Mwanakijiji |
| HAMISI MBWANA | - | Mwanakijiji |
| IDD Y. KIMBETE | - | Mjumbe S/Kijiji |
| BAKARIM. NGAIMA | - | Skauti |
| ALLY O. MNETE | - | Mjumbe S/Kijiji Mjumbe S/Kijiji |
| OMARY S. MALUKA | - | Mjumbe S/Kijiji |
| BAKARI S. MKUMBI | - | Mwanakijiji |
| MAHAMUDIM. MTAUKA | - | Mwanakijiji |

| |
|---|
| ZAINABUI. ROGORO - Mwanakijiji |
| MWANAHAWA O. MZIWANDA - Mwanakijiji |
| KHAMIS S. PONGWA - Mwanakijiji |
| BAKARI M. PELENGO - Mwanakijiji |
| ATHMAN O. MWERA - Mwanakijiji |
| ATHUMAN M. MTERUKA - Mwanakijiji |
| MAHAMUDI B. MAKUTIKA - Mjumbe/ k/Mazingira |
| YUSUF A. MNYACHIMO - Mjumbe K/Mazingira |
| RASHID H. MING'URO - Mjumbe S/Kijiji |
| MWICHACHE A. MKURUNGO - Mjumbe S/Kijiji |
| JABU A. KISOMA - Mjumbe S/Kijiji |
| FATUMA B. BING'URO - Mjumbe K/Mazingira |
| MOHAMED S. MPENGO - Mjumbe K/Mazingira |
| HASSAN Y. MKINGA - Mjumbe S/Kijiji |
| JUMANNE S. AMAGAE - Mjumbe S/Kijiji |
| MOHAMED O. MNYACHIMO - Mjumbe S/Kijiji |
| ILIHAMU A. MATIMBWA - Katibu K/Mazingira |
| MAFUZU M. JMZIWANDA - Mwanakijiji |
| SHAULI H. AMAGAE - Mwanakijiji |
| MOHAMED. S. MGOMI - Mwanakijiji |
| MAULID M. MZIWANDA - Mwanakijiji |
| RAJABU M. MNETE - Mwanakijiji |
| MOHAMED A. MPONGWA - Mwanakijiji |
| RASHID B. MG'OMBE - Mwenyekiti K/Mazingira |
| IDD Y. MAJKUTIKA - Mwanakijiji |
| BAKARI H. AMAGAE - Skauti na S/Kijiji |
| MOHAMED S. MNETE - Mjumbe K/Mazingira |
| SAID A. NGALIFUMBO - Mjumbe K/Mazingira |
| MWIDINI B. NGULANGWA - Mjumbe S/Kijiji |
| MARIAMU BAKARI - Mwanakijiji |
| ZAINA ALLY MING'URO - Mwanakijiji |
| SAID S. GUBALA - Mwanakijiji |
| ALLY HAMIS - Mwanakijiji |
| SHAURI S. MAKUTIKA - Mwanakijiji |
| AWAMIM. MZIWANDA - Mwanakijiji |
| SAID A. NGIMBU - Mwanakijiji |
| MAIMUNA RUMBONGO - Mwanakijiji |
| RUKIA O. LIMBALE - Mjumbe S/Kijiji |
| AHAMED M. KISOMA - Mwanakijiji |
| HUSUNA IDD MAKUTIKA - Mwanakijiji |
| MOHAMED H. MZIWANDA - Mwanakijiji |
| RAJAB IDD MAKUTIKA - Mwanakijiji |
| ATHUMAN K. KIONGA - Mganga wa Kienyeji |
| 100.ASHA KISOMA - Mwanakijiji |
| 101.PILI AMAGAE - Kamati Mboga na Matunda |
| MOHAMED M. MATOPE - Katibu Kamati ya Mikoko |
| MOHAMED S. NGATIAE - Bwana Nyuki wa Kijiji |
| MAULID R. KIGUMI - Bwana Mikoko wa Kijiji |
| JAFARI M. NGAIMA - Mwenyekiti Serikali ya Kijiji |
| JUMANNE KAPITAPO - Mwanakijiji |
| RAMADHAN R. CHAUGAMBO - Mwenyekiti wa Kitongoji |
| ALLY H. YELEU - Mwanakijiji |
| HAMIS I. TUNDUSI - Mwnakijiji |
| SAID JUMA GUBALA - Mwanakijiji |
| ABDULAHMAN Y. MNYACHIMO - Mwanakijiji |
| AHAMAD M. KISOMA - Mwanakijiji |
| MUHAMED A. MPOGO - Mwanakijiji |
| HAMIS M. JMCHAMBUKA - Mwanakijiji |

## 7.3 Kiambatanisho 'C'

**Muhtasari wa Utaratibu wa Kutunga Sheria Ndogo za Kuhifadhi Maliasili Vijijini**

**Utaratibu wa kutunga sheria ndogo za kuhifadhi maliasili (kama sheria ndogo nyingine) za vijiji umeelekezwa na Katiba, Sheria za Serikali za Mitaa, 1982, Sheria ya Ardhi Vijijini, 1999 na Sheria ya Tafsiri, 1996.**

Pamoja na kwamba sheria hizi hapo juu zimetoa mwelekeo wa utaratibu wa kutunga sheria ndogo, huu mwelekeo unabidi usomwe kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na kesi za Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa ambazo zimefafanua baadhi ya vipengele husika.

Kwa ujumla, zipo awamu kuu tatu katika zoezi zima la kutunga sheria ndogo za vijiji ambazo ni:

**Kabla ya Kutunga Sheria**

- Taarifa ya Mkutano: Kuna umuhimu wa kutoa taarifa ya mkutano wa kikao cha kujadili utunzi wa sheria ndogo kwenye Halmashauri Kuu ya Kijiji ambacho ndiyo chombo kilichopewa mamlaka ya kutunga sheria ndogo za kijiji. Taarifa hii inapaswa kutolewa angalau wiki moja na nusu kabla ya kufanyika mkutano.

  Katibu ndiye anayetoa taarifa ya mkutano wa Kijiji. Taarifa ieleze bayana siku, tarehe, saa na sehemu kikao kitakapofanyika.

Taarifa pia inabidi iambatanishwe na ieleze "agenda" ya mkutano. [Kwa mfano "agenda" ya kikao hiki itakuwa ni kutunga sheria ndogo ya kuhifadhi misitu na maliasili zote kwenye misitu iliyopo sehemu "X".]

- Mwanakijiji atakayeshindwa kuhudhuria, kwa kuwa hatakuwepo kijijini wakati wa mkutano anaweza kuwakilishwa na mwanakijiji mwingine kwa yeye kutoa taarifa ya maandishi (barua) kwa Katibu au Mwenyekiti wa Kijiji. Taarifa hii itakuwa inamruhusu mwakilishi kutoa maoni ya mwenzake ambaye hakuweza kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake. Katibu ataisome taarifa hii kwenye mkutano ili kuwajulisha wanakijiji wengine.

**Wakati wa Kutunga Sheria**

- Idadi ya wanaohitajiwa ili kupitisha sheria (Koram) iwe theluthi mbili.
- Wanaoruhusiwa kupiga kura wawe ni wanakijiji waliojiandikisha kama wanakijiji kufuatana na sheria, wawe na umri usiopungua miaka kumi na nane na wawe wenye akili timamu.
- Kikao cha kijiji kinabidi kifanyike na wanakijiji waliojiandikisha kama wanakijiji wa kijiji hicho. Wanaweza wakawepo waalikwa toka nje ya kijiji, lakini hawa hawaruhusiwi kupiga kura katika kufikia maamuzi.

**Adhabu za Sheria Ndogo**

- Faini itakayotozwa kwenye sheria ndogo isizidi shilligi elfu hamsini (Tshs 50,000:00)
- Pamoja na faini, sheria ndogo pia inaweza kuelekeza kwamba mali au vitu vilivyotumika katika kuvunja sheria vitaifishwe na viwe mali ya kijiji.
- Adhabu ya kifungo au kuadhibu kwa kuchapa viboko hairuhusiwi kuwepo kwenye sheria ndogo. Sheria ndogo itakayoenda kinyume na utaratibu huu wa adhabu itakuwa batili.

**Baada ya Kutunga Sheria**

1. Nakala za sheria ndogo zilizopendekezwa na wanavijiji pamoja na nakala ya muhtasari wa kikao/mkutano ulioidhinisha mapendekezo ya sheria hizo vinapaswa kupelekwa kwenye Halmashauri ya Wilaya ili kuidhinishwa. Ni vyema kupitisha mapendekezo ya

sheria hizo kwenye Kata ili kuchangia mawazo kuepuka uwezekano wa migongano na mapendekezo yo yote ya kijiji/vijiji jirani. Kata haina uwezo wa kubadilisha sheria za kijiji bali inaweza kutoa mapendekezo.

2. Baada ya kuridhika kuwa sheria ndogo za kijiji hazipingani na sheria Mama husika, basi Halmashauri ya Wilaya itaipa namba na itatangaza sheria hii kwenye Gazeti la Serikali ili kuwawezesha wananchi wachangie mawazo kwa muda uliowekwa. Iwapo sheria hizo hazitapingwa na mtu au taasisi yo yote ile katika kipindi kilichowekwa, basi zitakuwa sheria kama sheria nyingine yoyote ile ya nchi.

3. Katika zoezi hili, Halmashauri ya Wilaya inaweza ikapunguza au kuongeza baadhi ya vipengele vya sheria vilivyopendekezwa na kijiji ili kuvifanya viende sambamba na sheria Mama au na sheria nyingine husika.

Kijiji kinaweza kupata nakala ya sheria ndogo iliyopita kupitia kwenye ofisi za mwanasheria wa Halmashauri

## 7.4 Mapicha

Uchoraji ramani – skauti wa kikke wa Mbunju mvuleni anawaonyesha wakufunzi na Afisa Wanyamapori wa Wialya njia za tembo katika kijiji chake. Baadhi ya waliohudhuria masomo.







